CHAMA CHA MAPINDUZI
WILAYA YA LONGIDO

OFISI KUU YA WILAYA * S. L. P 4 LONGIDO *
SIMU NA. 0784-957 504
Barua zote ziandikwe kwa katibu wa CCM Wilaya.

TAARIFA KWA UMMA

HATI YA TAMKO LA KAMATI YA SIASA WILAYA YA LONGIDO JUU YA UHARIBIFU WA MIUNDO MBINU YA MAJI LEO TAREHE 19.10.2026

Kamati ya siasa ya Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Longido, imekutana kwa dharura kwa ajili ya kupata taarifa juu ya ukosefu mkubwa wa maji katika Wilaya ya Longido hususan katika mji wa longido na Namanga ambayo ni maeneo yenye mkusanyiko mkubwa na yanayotegemea maji ya mto simba na kuagiza yafuatayo;

1. Kamati ya Siasa imemtaka Mkuu wa Wilaya ya Longido kuhakikisha watu wote waliohusika katika kuhujumu miundo mbinu ya maji ya katika bomba litoalo maji kutoka mto simba, wanakamatwa na kuwajibika ipasavyo kwa kusababishia Serikali Hasara na kuwaletea wananchi wa maeneo yanayotegemea maji hayo usumbufu mkubwa wa upatikanaji wa maji kwa watu na mifugo.

2. Kamati ya Siasa pia, imemtaka mkuu wa Wilaya, kuhakikisha watu hao watakapopatikana wafikishwe kwenye vyombo vya sheria kwa ajili ya uwajibikaji zaidi

3. Kamati ya Siasa imeshauri kuwa, viongozi wa maeneo ambayo uharibifu wa bomba la maji umekuwa ukijirudia, wawajibike kutoa ulinzi juu ya bomba hilo na kutoa taarifa mara kwa mara kwa Mkuu wa Wilaya juu ya usalama wa bomba hilo

4. Kamati ya Siasa inawaomba wananchi kuwa walinzi wa miundo mbinu muhimu ya maji na kutoisababishia Serikali Hasara kubwa Matika mradi huo mkubwa na ulioigharimu serikali fedha nyingi mpaka kukamilika

Kidumu Chama Cha Mapinduzi

Solomon Lekui
Katibu wa siasa, Uenezi na Mafunzo
Wilaya ya Longido